# MKATABA WA UTARATIBU WA RIDHAA YA MAPEMA KWA BAADHI YA KEMIKALI HATARISHI ZA VIWANDANI NA VIUATILIFU KATIKA BIASHARA YA KIMATAIFA (*Rotterdam Convention on the Prior Informed Consent Procedure for Certain Hazardous Chemicals and Pesticides in International Trade)*

## 1. UTANGULIZI

Mkataba wa Utaratibu wa Ridhaa ya Mapema kwa Baadhi ya Kemikali Hatarishi katika Biashara ya Kimataifa (***Rotterdam Convention on the Prior Informed Consent Procedure for Certain Hazardous Chemicals and Pesticides in International Trade)*** ni mkataba wa kimataifa unaolenga kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya athari hatarishi za kemikali na viuatilifu hatarishi katika biashara ya kimataifa. Mkataba wa Rotterdam ulipitishwa rasmi katika mkutano wa kidiplomasia uliofanyika Rotterdam tarehe 10 Septemba, 1998 na ukaanza kutumika rasmi tarehe 24 Februari, 2004.

Tanzania ni nchi mwanachama wa Mkataba wa Rotterdam kuhusu upashanaji taarifa ya kemikali hatarishi za viwandani na viuatilifu katika biashara ya kimataifa Mkataba wa Rotterdam ulipitishwa huko Rotterdam (Uholanzi) ambao unalenga kukuza uwajibikaji wa pamoja kuhusiana na biashara ya kimataifa ya kemikali hatarishi. Tanzania iliridhia Mkataba huu mwaka 2004. Mkataba huu unasimamiwa na kutekelezwa kwa pamoja na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) na Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA).

Nchi wanachama wa Mkataba zinapaswa kubadilishana taarifa kuhusu madhara ya kemikali zinazodhibitiwa chini ya Mkataba huu ili kuziwezesha nchi hizo kufanya maamuzi ya kukubali aidha kuziingiza katika nchi husika au kuzisafirisha nje ya nchi. (Export and import decisions). Mkataba huu unahakikisha kuwa nchi zinapokea taarifa kamili na kutoa idhini ya awali (Prior Informed Consent – PIC) kabla ya kuingiza kemikali au viuatilifu vilivyoainishwa kuwa hatarishi. Lengo lake kuu ni kukuza uwajibikaji wa pamoja na utoaji wa taarifa kati ya nchi zinazouza na zinazonunua kemikali hizo.

## 2. MALENGO YA MKATABA

Lengo kuu la Mkataba huu ni kuimarisha jitihada za jumuiya ya kimataifa katika kudhibiti uzalishaji na biashara ya kemikali hatarishi kwa ajili ya kulinda afya ya binadamu na mazingira.

Malengo mahsusi ni pamoja na:

i) Kuhakikisha kunakuwepo na uwajibikaji na ushirikiano wa pamoja katika biashara ya Kimataifa kwa baadhi ya kemikali hatarishi na viuwatilifu;
ii) Kukuza uwajibikaji wa pamoja katika biashara ya kimataifa ya kemikali hatarishi zenye madhara kwa binadamu na mazingira yake;
iii) Kubadilishana taarifa kuhusu sifa za kemikali ambazo wahusika katika mkataba huu wanafanya biashara ili kuchangia katika matumizi mazuri ya kimazingira ya kemikali hizo.

## 3. USHIRIKI WA MIKUTANO

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hushiriki katika mikutano chini ya Mkataba wa Rotterdam ambayo hufanyika kila baada ya miaka miwili katika ngazi za kimataifa na kikanda. Mkutano wa Nchi Wanachama (Conference of the Parties – COP) hufanyika kujadili sera, marekebisho na maamuzi ya utekelezaji wa mkataba.

Aidha, Mikutano ya Kamati ya Uzingatiaji (Compliance Committee) hufanyika kujadili na kupitia masuala ya kimfumo yanayohusu uzingatiaji wa jumla wa Mkataba wa Rotterdam, yakiwemo utekelezaji wa sheria, sera na taratibu za kitaifa, taarifa za hatua za mwisho za kisheria, pamoja na masuala ya uingizaji na usafirishaji wa kemikali zilizoainishwa katika Kiambatisho cha III cha Mkataba. Vilevile, Mikutano ya Kamati ya Mapitio ya Kemikali (Chemical Review Committee – CRC) hufanyika kujadili na kupitia maombi mapya ya kemikali na kupendekeza kemikali mpya ziingizwe kwenye kiambatisho III. Vilevile, kuchambua madhara ya kemikali zilizopendekezwa kwa afya ya binadamu na mazingira.

## 4. MAJUKUMU YA NCHI WANACHAMA

Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Mkataba wa Rotterdam, Kupitia ushiriki huu, Tanzania huchangia katika maamuzi ya kimataifa na kuimarisha udhibiti wa biashara ya kemikali na hutekeleza mkataba huu kupitia:

- Uteuzi wa Mamlaka Teule ya Kitaifa (*Designated National Authorities-DNA*) kwa ajili ya kuratibu utekelezaji.

- Uanzishaji na utekelezaji wa sheria na kanuni za usimamizi wa kemikali na viuatilifu, ikihusisha taasisi kama NEMC, TPHPA, GCLA, OSHA na TRA.
- Ushiriki katika mikutano ya kimataifa ya COP, CRC na Kamati ya Uzingatiaji.
- Utoaji wa taarifa za kitaifa kuhusu udhibiti wa kemikali hatarishi na utekelezaji wa PIC.

## 5. FAIDA ZA MKATABA

- Mfumo wa onyo la mapema: kupitia PIC Circular inayotolewa kila baada ya miezi sita, Nchi Wanachama hupata taarifa za mapema kuhusu marufuku ya kitaifa au vizuizi vikali vilivyowekwa na Nchi nyingine kwa kemikali hatarishi. Pia hupokea taarifa juu ya matukio ya madhara yaliyosababishwa na matumizi ya mchanganyiko wa viuatilifu hatari, kama vile sumu kwa binadamu au uharibifu wa mazingira.

- Maamuzi yenye taarifa: Nchi Wanachama hupokea hati ya mwongozo wa kufanya maamuzi (Decision Guidance Document — DGD) kwa kila kemikali iliyo kwenye Nyongeza III ya Mkataba. Taarifa zilizomo kwenye DGD hutoa msingi wa kufanya maamuzi sahihi kuhusu kuagiza au kutoagiza kemikali hizo katika siku zijazo.

- Uwajibikaji wa pamoja: Mkataba unasaidia Nchi Wanachama kusimamia vizuri zaidi kemikali na kuepuka uingizaji wa kemikali zisizohitajika, kwa kukuza uwajibikaji wa pamoja kati ya nchi zinazoagiza na zinazouza. Nchi zinazoagiza zina jukumu la kufanya maamuzi yenye taarifa kwa wakati kuhusu uagizaji wa baadaye, huku nchi zinazouza zina jukumu la kuhakikisha kuwa mauzo hayafanyiki kinyume na maamuzi ya uagizaji yaliyotolewa na nchi zinazoagiza.

- Kusaidia kudhibiti kemikali zisizotakiwa kuingizwa nchini.

- Kusaidia kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu.

## 6. MAFANIKIO YA MKATABA

- Nchi hushiriki katika warsha za kujengewa uwezo kuhusu usimamizi na udhibiti wa kemikali;
- Kusaidia kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu;
- Kusaidia kubadilishana taarifa za awali kuhusu kemikali hatarishi za viwandani na viuatilifu katika biashara ya kimataifa.

- Kuandaa *National Implementation Plan* (NIP) na kuwasilishwa Sekretarieti ya mkataba;
- Kupata taarifa kuhusu kemikali hatarishi za viwandani na viuatilifu katika biashara ya kimataifa;
- Kuweza kudhibiti kemikali zisizotakiwa kuingizwa nchini;

## 7. CHANGAMOTO ZINAZOKABILI UTEKELEZAJI WA MKATABA

- Usafirishaji haramu wa kemikali hatarishi.
- Kukosekana kwa taarifa muhimu kuhusu kemikali zinazosafirishwa nchi mbalimbali.
- Baadhi ya nchi kuchelewa au kutokutoa kabisa idhini ya kupokea taka zinazosafirishwa nje ya nchi.
- Baadhi ya nchi kutoridhia au kuchelewa kuridhia baadhi kemikali kuorodheshwa kwenye kiambatisho (Annex) cha kemikali zinazodhibitiwa chini ya Mkataba.